

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BUNGE LA TANZANIA**

*Simu:* +255 026 23222761-5  
*Fax No.* +255 026 2322624  
**E-mail:** [cna@bunge.go.tz](mailto:cna@bunge.go.tz)



Ofisi ya Bunge,  
S.L.P. 941,  
**DODOMA**

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

---

Vikao vya Kamati 14 za Kudumu za Bunge vitaanza Jumatatu tarehe 22 Oktoba na kuendelea hadi tarehe 04 Novemba 2018, Jijini Dodoma. Shughuli zote za Kamati katika kipindi hicho zimepangwa kwa kuzingatia Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016. Shughuli hizo ni kama ifuatavyo:-

- (i) Uchambuzi wa Taarifa mbalimbali za Msajili wa Hazina kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma katika Mashirika na Taasisi mbalimbali Nchini.
- (ii) Uchambuzi wa Taarifa ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Hesabu zilizokaguliwa za Serikali Kuu za Mwaka 2016/2017
- (iii) Uchambuzi wa Taarifa ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Hesabu zilizokaguliwa za Serikali za Mitaa za Mwaka 2016/2017.
- (iv) Uchambuzi wa Taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali.
- (v) Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa tarehe 10 Septemba, 2018 wakati wa Mkutano wa Kumi na Mbili wa Bunge.

Ratiba zote za Shughuli za Kamati za Bunge zinapatikana katika Tovuti ya Bunge ambayo ni [www.parliament.go.tz](http://www.parliament.go.tz).

**Imetolewa na:** Kitengo cha Habari, Elimu kwa Umma na Mawasiliano  
Ofisi ya Bunge  
**DODOMA**  
12 Oktoba, 2018